



TUMERITHI TUWARITHISHE



Kampeni ya kuboresha Utunzaji wa Misitu

Misitu ni rasilimali ambayo ina mchango mkubwa katika maisha ya Watanzania wengi lakini matumizi mabaya ya misitu na yaliyopitiliza pamoja na utawala mbovu yanatishia uwepo wa misitu hiyo na mchango wake katika maendeleo. Ripoti ya Mwaka 2007¹ imeonyesha mapungufu makubwa katika biashara ya mbao hususani katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Kampeni ya Mama Misitu inalenga kutatua mapungufu hayo kwa kuboresha utawala na utunzaji wa misitu ili Watanzania waweze kunufaika zaidi kutokana na utunzaji endelevu wa misitu. Kampeni hii ilizinduliwa na Kikundi Kazi Cha Masuala ya Misitu Tanzania kinachoratibiwa na Jumuiiko la Maliasili Tanzania kwa lengo la kufanya majaribio mnamo Mwaka 2008. Mwaka 2012, kampeni ya Mama Misitu imezindua mpango wa miaka mitano ili kufikia jamii nyingi zaidi kutokana na uzoefu na mafunzo yaliyopatikana katika kampeni ya awali.



¹ Milledge, S.A.H., Gelvas, I.K. and Ahrends, A.2007. *Forestry, governance and national development: Lessons learned from a logging boom in southern Tanzania*. TRAFFIC East & Southern Africa/ Tanzania Development Partners Group/Ministry of Natural Resources of Tourism, Dar es Salaam

Mafunzo yaliyotokana na kampeni ya awali

Kampeni ya Mama Misitu ilitekelezwa katika wilaya za Rufiji na Kilwa na ilifanikiwa kutatua vikwazo mbalimbali ikiwemo utawala na utunzaji wa misitu ili kujikimu kimaisha. Kwa kupitia kampeni hii, jamii imeweza kujifunza sheria zinazohusiana na uvunaji wa mbao, nafasi ya serikali katika kutunga sheria na kuzisimamia ili kulinda rasilimali misitu, thamani ya mazao ya misitu yaliyovunwa kihalali na yale yasiyovunwa kihalali na jinsi ya kuwashughulikia majangili wa misitu na kuwapeleka mbele ya sheria.

Hivyo kampeni ya Mama Misitu inatarajia kutanua wigo wake wa utekelezaji kutokana na uzoefu uliyopatikana katika kampeni ya awali ili kuweza kufikia jamii nyingi zaidi.



Kukuza malengo na matokeo

Kampeni mpya ya Mama Misitu ya miaka mitano itazinduliwa katika wilaya nne (4) ambazo ni Rufiji, Kilwa, Kisarawe na Kibaha kabla ya kuongezeka na kufikia jumla ya wilaya nane (8). Washiriki kumi na moja (11) wataitekeleza kampeni hii katika ngazi za wilaya na kitaifa. Watekelezaji katika ngazi ya kitaifa ni; LEAT, TNRF, Femina HIP, MJUMITA, JET, Policy Forum na TRAFFIC. Watekelezaji katika ngazi ya wilaya ni, TFCG, MCDI, WWF, WCST². Katika kila wilaya hizo, kampeni hii itaongeza uelewa na kuboresha mbinu za utunzaji wa misitu katika jamii.

Kampeni ya Mama Misitu kupitia wabia wake imeweza kutambua changamoto katika utawala wa misitu ambayo ingependa kushughulikia matatizo yafuatayo:

- Wananchi kutofahamu haki na wajibu wao katika masuala ya misitu
- Utekelezaji hafifu wa sera na sheria mbalimbali zinazohusu usimamizi wa rasilimali misitu
- Usimamizi mbovu wa sheria za ardhi
- Udhhibiti mbovu wa sekta ya biashara; pamoja na
- Kuwepo kwa udanganyifu mwingi katika mnyororo mzima wa biashara ya mbao katika ngazi mbalimbali.

Kampeni ya Kitaifa yenye muktadha toka kwa jamii

Wanajamii wanapaswa kunufaika na rasilimali za misitu na kwa sababu hii mawazo yao ndiyo kiini cha kampeni hii. Kijitabu hiki kinajumuisha shuhuda kutoka katika jamii kuhusu manufaa na vikwazo katika kuboresha utawala wa rasilimali misitu nchini Tanzania.





Bwana Omari Kijumile ni mzawa na mkulima katika kijiji cha Ruhatwe kilicho katika wilaya ya Kilwa. Amehusika na kampeni ya Mama Misitu kutoka mwanzo ambapo wataalamu walifika na kutoa mafunzo na kuwaelimisha watu mambo mbalimbali kuhusu sera na sheria ambazo zinahusika katika utunzaji wa misitu Tanzania. Mfano, Sera ya Misitu ya mwaka 1998, Sheria ya Misitu ya mwaka 2002, Sheria ya Ardhi ya mwaka 1998 na 1999 pamoja na Sera ya Mazingira ya mwaka 2004. Vifaa vilivyokuwa vikitumika wakati wa kampeni hiyo vilijumuisha maigizo, mashairi na ngoma za asili.

Kutokana na hilo kuna mafanikio mengi yamejitokeza kwenye hizi hatua za mwanzo tu za Mama Misitu. Kumekuwa na ongezeko kubwa la jamii kujihusisha ili kujua namna na umuhimu wa miti na misitu na sera na sheria zinazotumika kulinda utunzaji wa mazingira. Jamii imefahamishwa juu ya ukataji miti unaopelekea kuongezeka kwa ukame, kupata mvua kidogo za msimu au kupata mafuriko pindi mvua zinyeshapo na mabadiliko ya hali ya hewa ingawa zinabaki kama changamoto. Changamoto ya muhimu iliyotajwa na Bw. Omari ilikuwa ni mgongano uliopo kati ya sera ya Kilimo Kwanza na utunzaji wa misitu. Kinachotokea ni kwamba jamii inaangalia kilimo kama inavyohamasishwa na sera za Kilimo Kwanza ikimaanisha ukataji wa miti na misitu inayotakiwa kuhifadhiwa ili kupisha shughuli za kilimo.





Mama Mwanisha Abdallah Likoko ni mzawa katika kijiji cha Kikole wilayani Kilwa. Ameshuhudia mabadiliko aliyoyaona katika kijiji chake kwa jinsi ambavyo misitu inahifadhiwa. Hapo mwanzoni miti na misitu ilikuwa ikikatwa sana na hakukuwa na aliyekuwa akijishughulisha na shughuli hizi kuona ni nini kinakatwa na kinapandwa na ni nani aliyekuwa akikata miti. Mabadiliko anayoyaona sasa Mwanisha ni kuwa miti inakatwa kwa kufuata sheria na utaratibu uliopo wa uhifadhi misitu. Ameweza pia kuchangia katika mabadiliko katika misitu ambayo yameletwa na kampeni ya Mama Misitu. Kwa sasa ana matumaini kuwa vizazi vijavyo vitakuta misitu na miti minene.

Mwanisha alieleza kuwa jamii kubwa ya watu wana ufahamu na uelewa juu ya umuhimu wa miti na misitu ingawa kuna baadhi ya watu wanaokataa kusikiliza na kuelewa na pia anaona changamoto inayowakuta wanawake katika suala hili la utunzaji wa misitu. Wanawake wanaathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na miti na misitu. Mwanisha alieleza kuwa wanawake wanaelewa kwa haraka umuhimu wa miti katika kuleta mvua, vyanzo vya maji na kadhalika lakini wanaume ni watu wa kutafuta fedha kwa hiyo wanaangalia miti kama chanzo cha wao kupata fedha na hivyo hawatakubaliana na suala la kuhifadhi misitu kama ambavyo wanawake wanafanya. Hivyo kuna umuhimu wa kuongeza mkazo zaidi kwa wanaume juu ya uhifadhi wa misitu kwa jamii.



Bwana Mwalami Ali Kwangaya ni mzawa wa Rufiji na Katibu Muhtasi wa mtandao wa kuhifadhi misitu kijijini kwake. Anashuhudia kuwa kabla ya kampeni ya Mama Misitu jamii haikujua kuwa misitu na miti ni mali yao. Hivyo bila kuelewa suala hilo hawakuona umuhimu wa kuhifadhi miti na misitu husika. Kampeni ya Mama Misitu kutumia nyimbo, maigizo na sanaa imewasaidia wanajamii kuona athari za ukataji miti uliopitiliza ikiwa ni pamoja na kupotea kwa wanyama, ukame na mabadiliko ya hali ya hewa, hivyo wamebadilisha njia zao za utafutaji wa kipato kutoka ukataji wa miti ili kutengeneza mkaa na badala yake kuunda vikundi mbalimbali vyenye shughuli mbalimbali za kujipatia kipato ambazo hazihusiani na uharibifu wa misitu.

Mbali na hayo, Bwana Mwalami anaeleza kuwa misitu inapatwa na changamoto kama kuvamia misitu kutokana na udhaifu wa ulinzi katika njia mbalimbali za kuingilia misituni. Kuna umuhimu mkubwa kuwa serikali inabidi kutenga fedha kwa ajili ya ulinzi katika misitu, milango madhubuti na ulinzi dhabiti pamoja na nyenzo mbalimbali za ulinzi ni muhimu. Pia, kunahitajika msaada wa kifedha kutoka serikalini ili kudhibiti makundi hayo kuamua kuingia misituni kujikatia miti ili kupata kipato pindi wakwamapo. Kwa hiyo mkazo utolewe katika uendelezaji wa shughuli zingine za kujipatia kipato.







Jumuiko
la
Maliasili
Tanzania



Tanzania
Natural
Resource
Forum



TRAFFIC
the wildlife trade monitoring network



www.mamamistu.org

Kampeni ya Mama Misitu inapokea msaada toka Serikali ya Finland na Norway.



MINISTRY FOR FOREIGN
AFFAIRS OF FINLAND



NORWEGIAN EMBASSY